

jana. Kushoto ni Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe. (Picha na Iddy Mwema).

HABARI LEO UK 8

* Wizara yaandaa mkakati kudhibiti uvuvi haramu *

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi kwa kuhirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) imeandaa mkakati wa muda mfupi na muda mrefu wa kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu nchini.

Utekelezaji wa mkakati huo utashirikisha viongozi wa ngazi za vijiji, kata, tarafa, wilaya na mikoa ili kudhibiti matumizi ya zana haramu ikiwemo nyavu zenye matundu madogo na kokoro.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alisema hayo wakati akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalumu, Aleksia Kamguna (CCM) aliyetaka kufahamu serikali ilivyojipanga

kukomesha uvuvi haramu wa kuvua samaki kwa kutumia nyavu zenye matundu madogo.

"Serikali inaboresha mfumo wa utoaji wa vibali vya kuingiza zana za uvuvi nchini ili kudhibiti uingizwaji wa zana haramu ikiwemo nyavu zenye matundu madogo na makokoro," alisema Ulega.

Alisema serikali inaendelea kuimarisha shughuli za ukaguzi wa zana za uvuvi zinazoingizwa nchini kupitia njia za mipakani na bandarini kwa kuongeza idadi ya watumishi na vitendea kazi.

"Hili litaongeza wigo wa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo ya mipakani na bandarini... serikali itaendelea kutoa elimu kwa wavuvi, wain-

gizaji na wasambazaji wa zana za uvuvi pamoja na jamii kwa ujumla kuhusu athari za matumizi ya zana haramu za uvuvi," alisema na kutaja miongoni mwake ni nyavu zenye matundu madogo, kokoro na matumizi ya vilipuzi.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalumu, Christine Ishengoma (CCM) alitaka kufahamu mkakati wa serikali kuhamasisha wanaoleta nyavu, wakaanzisha viwanda nchini kutengeneza nyavu zinazotakiwa.

Ulega alisema: "Tumeshaanza kupata viwanda vipya vya kutengeneza nyavu na Mwanza kipo kipya cha Ziwa Net. Tuna maombi pia ya uwekezaji kwenye eneo hili."

Big Solutions Company Ltd managing director Rajab Mchatta (C) briefs journalists in Dar es Salaam yesterday on the Tanzania Photographers and Videographers Forum meeting scheduled to be held in the city on June 6. He is flanked by one of the forum's instructors, Hanif Abdulrasul (L), and forum sponsor Haika Lawele. Photo: John Badi

THE GUARDIAN Pg. 4

Govt to improve systems for issuance of permits to import fishing equipment

By Getrude Mhago, Dodoma

THE government is improving systems on issuance of permits to import fishing gear so as to control importation and sale of illegal tools including unpermitted fishing nets, the National Assembly heard yesterday.

It has also continued to strengthen patrol and inspection of fishing tools imported into the country through borders posts and ports as well as by increasing the number of

employees and modern tools.

Minister for Livestock and Fisheries Abdallah Ulega told legislators when responding to a question by Aleksia Kamunga (Special Seats) who wanted to know the government's plans to control illegal fishing, specifically those who are using illegal fishing nets thus affecting production of fish in the country's oceans and lakes.

According to him, the ministry in collaboration with various stakeholders including the

President's Office, Regional Administration and Local Government (PORALG) has prepared a short and long term plan to fight illegal fishing in the country.

"The implementation of the strategy will involve leaders in villages, wards, divisions, districts and regions to control the use of illegal tools in fishing including nets that are prohibited," he said.

He further said the government will also continue providing education to fishermen, importers

and distributors of fishing gear as well as the general on the effects of using illegal gear such as nets and explosives in fishing.

The minister further said the ministry will also continue investing in patrol, monitoring and surveillance in Lakes, ocean and rivers to curb illegal fishing.

He insisted that the fight against illegal fishing was endless, urging those engaging in the activity to adhere to the country's laws.

The 2017 report by the Food and Agriculture Organisation (FAO) said illegal fishing was still rampant in the western Indian Ocean coast, causing Tanzania an annual loss of \$400 million.

siku tatu zilizopita. Hiyo ilikuwa Juni, 1988.

TAFAKURI

UHURU UK 6.

Wanawake changamkieni fursa katika uvuvi, ufugaji wa samaki

KILIMO ni uti wa mgongo wa taifa, hilo linatokana na ukweli kwamba asilimia kubwa ya wananchi hutegemea kilimo kama kazi ya msingi ya kiuchumi inayowaingizia kipato.

Wanawake ni miongoni mwa wananchi hao ambapo mbali na kujihusisha na kilimo, pia wapo wanaojihusisha na uvuvi na ufugaji wa samaki.

Hivi karibuni wizara ya Mifugo na Uvuvi ilisema katika mwaka wa fedha 2022/2023, kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), ilitekeleza mradi wa kutoa mikopo yenye masharti nafuu na isiyo na riba, ya pembejeo za ufugaji samaki ikijumuisha vizimba kwa wanufaika 3,154.

Ilielezwa kwamba, mikopo hiyo inahusisha vifaranga na chakula cha samaki kwa lengo la kuwawezesha wafugaji kufuga kwa njia ya vizimba.

Naibu Waziri wa Kilimo na Uvuvi, David Silinde, akizungumzia maendeleo ya sekta ya uvuvi alisema wanufaika 3,154 wameainishwa kunufaika na mradi huo vikijumuishwa vikundi 93, kampuni 10 na watu binafsi 32.

Kwa upande wa Halmashauri ya Mji wa Geita, vikundi vitatu vinatarajiwa kunufaika na programu hiyo kikiwemo kikundi cha Tumaini, chenye wanachama 10 kutoka Jimbo la Busanda ambapo wamepewa mikopo ya pembejeo za samaki katika vizimba vyenye thamani ya sh. milioni 69.4 kwa kila kikundi.

Kwa mujibu wa Silinde, katika mwaka wa fedha 2023/2024, serikali itaendelea kutekeleza mradi wa kutoa mikopo yenye masharti nafuu na isiyo na riba ya pembejeo

za ufugaji samaki kuwawezesha ufugaji katika vizimba 893.

Naipongeza serikali kwa kuendelea kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Uwezeshaji wa wananchi ni pamoja na kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi ikiwa sehemu ya

Ni matumaini
yangu kuwa,
miongoni mwa
watakaonufaika
na mkopo huo
wa pembejeo za
ufugaji wa samaki ni
wanawake ambao
kwa asilimia kubwa
wamejikita katika
sekta ya kilimo na
ufugaji hususani wa
samaki.

utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa kufikia mwaka 2025.

Ni matumaini yangu kuwa, miongoni mwa watakaonufaika na mkopo huo wa pembejeo za ufugaji wa samaki ni wanawake ambao kwa asilimia kubwa wamejikita katika sekta ya kilimo na ufugaji hususani wa samaki.

Aidha, kwa upande wa wanawake wanaojishughulisha na ufugaji, sasa ni wakati wenu



NA REHEMA MOHAMED

kuchangamkia fursa hiyo kwa kujiunga katika vikundi na kuanzisha vyama vya ushirika wa ufugaji samaki katika maeneo yatakayolengwa.

Pia, kupitia majukwaa ya uwezeshaji kiuchumi, wanawake wanaweza kujiunga katika vikundi na kuchangamkia mkopo huo uwawezeshe kuanzisha ufugaji wa samaki, kuimarisha hali zao na familia zao kiuchumi.

Wanawake wanapaswa kuchangamkia fursa hii kwa sababu soko la samaki linapatikana kwa urahisi nchini kutokana na matumizi yake kama kitoweo ndani na nje ya nchi.

Jambo kubwa katika uchukuaaji wa mikopo hii ni kuzingatia uaminifu na kurejeshaji kwa wakati lengo likiwa kutoa fursa ya kuwawezesha wananchi wengine kupata fursa ya kukopeshwa.

Wakati serikali ikistahili pongezi kutokana na hatua mbalimbali inazozichukua katika kuimarisha uchumi wa wanawake kupitia uvuvi na ufugaji, pia ni muda mwafaka kwa wadau wa maendeleo kuiunga mkono serikali katika kuwawezesha wananchi kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo kukuza uchumi wananchi na taifa kwa ujumla.